

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA MAKAMU WA RAIS

### TAARIFA KWA UMMA

Kutangaza washindi wa Shindano la Insha kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira

Dodoma, 19 Juni 2020.

Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau wa Mazingira iliandaa mashindano ya uandishi wa insha kuhusu masuala ya Mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Lengo la mashindano hayo ni kukuza uelewa na kuhamasisha ubunifu kwa wanafunzi na vijana katika masuala ya hifadhi ya mazingira.

Ofisi ya Makamu wa Rais inawashukuru wote waliojitokeza katika uandishi wa Insha hizo. Taratibu za kuwapata washindi zitakapokamilika, majina ya washindi na utaratibu wa ugawaji wa zawadi utatangazwa rasmi kupitia tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais yaani [www.vpo.go.tz](http://www.vpo.go.tz), vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali wasiliana na Bw. Enock Sanga kupitia simu namba 0753 326 234 au Bi. Martha Ngalowera - 0784 589 610.

Tangazo hili limetolewa na:

A blue ink signature of Lulu Mussa.

Lulu Mussa

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**